SAMPULI
Kuhusiana na COVID-19
Ombi la Nyumba Inayofaa

[Tarehe] _____
[Jina la Mwenye Nyumba] _____
[Anwani ya Mwenye Nyumba] _____
Tuma kupitia barua pepe: _____ **[anwani ya barua pepe]**

Kuh: Ombi la Nyumba Inayofaa

Mpendwa :_____

Mimi mpangaji wako wa nyumba katika _____ **[anwani].** Ninaandika ili kuomba nyumba inayofaa kwa sababu ya ulemavu.
Nina: **[teua chaguo zinazofaa]**

☐ ulemavu, unaolezwa na Sheria ya Haki ya Nyumba (Fair Housing Act) kama matatizo ya kimwili au kiakili ambayo yanamzuia mtu kutekeleza shughuli moja au zaidi muhimu za maisha (42 U.S.C. 3602(h)) ambao unaniweka katika hatari kubwa ya kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19. Lazima nipunguze shughuli zinazoweza kuniweka katika hatari ya kuambukizwa.

☐ matatizo ya kimatibabu ya kihisia au kimwili yanayoweza kutambulika au kubainishwa yanayolindwa na kifungu cha RCW 49.60.040 (7). Lazima nipunguze shughuli zinazoweza kuniweka katika hatari ya kuambukizwa.

Kama nyumba inayofaa, tafadhali:
[teua chaguo zinazofaa]

◇ Komesha ukaguzi usio wa dharura wa chumba changu ninakoishi kwa sababu ni hatari kwa afya yangu.

◇ Ondoa sera ifuatao ambayo siwezi kuifuata kwa sababu ya janga la COVID-19:
_____.

◇ Ongeza muda wa mwisho wa_____ambao siwezi kuutimiza kwa sababu ya janga hadi _____ **[tarehe ya baadaye]**

◇ Niruhusu nilipe kodi yangu ya nyumba kwa kuituma bila kutoza ada za kuchelewa kwa siku_____**[idadi]** baada ya tarehe ya kawaida ya muda wa mwisho wa kulipa. Siwezi kuondoka nyumbani kwangu ili kwenda kulipa kodi ya nyumba moja kwa moja kama kawaida.

◇ Wasiliana na_____**[jina],** ambaye atakuwa anashughulikia masuala yangu wakati nikiwa mgonjwa.

◇ Niruhusu niweke mkataba wa mpango wa malipo ili kupanga malipo ya kodi ya mwezi wa **[mwezi]** na uondoe (utoe msahama) ada zozote za kuchelewa.

◇ Lingine: _____

Maombi ya Nyumba Inayofaa

Mkazi mwenye ulemavu ambao unamfanya awe katika hatari zaidi ya kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19 anaweza kuomba nyumba inayofaa ili kupunguza uwezekano wa kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19.

Kwa mfano:

- Mkazi anaweza kuomba kutumia chumba cha kuosha nguo mara moja baada ya kusafishwa, au wakati wakazi wengine hawapo.
- Kuomba kucheleweshwa kwa ukaguzi wa kawaida wa chumba chake cha kuishi, au kutuma picha au video za chumba badala ya kufanyiwa ukaguzi wa moja kwa moja.
- Kuomba mwenye nyumba kupunguza idadi ya wafanyakazi wanaoingia chumbani ili kufanya ukarabati, na kuwahitaji wavae barakoa.
- Kuomba mtoa huduma za nyumba aonyeshe nyumba ambayo mpangaji atakuwa anahama kwa mpangaji mmoja mtarajiwa kwa wakati mmoja.

Watu wenye ulemavu wanaweza kuhitaji nyumba zinazofaa zisizo na kanuni zilizowekwa na mtoa huduma za nyumba kwa sababu ya ugonjwa wa COVID 19.

Kwa mfano:

- Watu wenye ulemavu wanaopokea huduma za mhudumu wa kibinafsi wana haki ya kuendelea kutembelewa na wahudumu wao, hata kama jengo wanakoishi haliruhusu wageni, au lina sera ya kudhibiti idadi ya wageni wanaowatembelea.

NORTHWEST FAIR HOUSING ALLIANCE
35 W. Main Ave., Suite 250, Spokane, WA 99201
Nambari ya simu: (509)-325-2665 / 1-800-FAIR (3247)
FAKSI: -866-376-6308 / www.nwfairhouse.org

Huduma zetu ni za bure.

Kazi iliyotoa msingi wa chapisho hili iliendelezwa kwa sehemu na ufadhili chini ya ruzuku kutoka kwa Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Miji ya Marekani (U.S. Department of Housing and Urban Development). NWFHA inawajibikaji kikamilifu kwa usahihi wa taarifa na ufafanuzi ulio kwenye chapisho hili.
Januari. 2021
Swahili

Haki za Nyumba kwa Makundi ya Watu Wanaolindwa walioathiriwa vibaya zaidi na janga la COVID 19

NORTHWEST FAIR HOUSING ALLIANCE

"Kujitahidi ili kuhakikisha nyumba sawa kwa wote"

(509)-325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
www.nwfairhouse.org

Athari za ugonjwa na vifo vinavyotokana na ugonjwa wa COVID-19 hazijaathiri watu wote kwa usawa katika Jimbo la Washington. Hali ya viwango vya juu na/ au kuwa na dalili kali zaidi kutokana na ugonjwa wa COVID 19 kati ya **Walatino, Waeshia na Wakazi wa Kisiwa cha Pasifiki, Waafrika, Wenyeji, watu wasio wazungu, na watu wenye ulemavu** katika eneo letu zinaongeza hatari yao ya kukumbwa na uabaguzi wa nyumba au kupoteza nyumba.

Sheria ya Haki ya Nyumba ya serikali inawalinda wanaotuma maombi ya kupanga nyumba, wapangaji, wenye nyumba na wanunuzi watarajiwa wa nyumba kutokana na kubaguliwa kwa msingi wa **asili, rangi, dini, jinsia, utaifa, hali ya familia** au **ulemavu**.

Kando na hayo, **Sheria ya Kupinga Ubaguzi ya Jimbo la Washington**(WLAD, Washington State Law Against Discrimination, RCW 49.60) inapinga ubaguzi wa nyumba kwa msingi wa **hali ya uanajeshi au mwanajeshi aliyestaafu, imani, hali ya ndoa, mwelekeo ya kuvutiwa kimapenzi**, na **hali ya uhamiaji au uraia**.

Hii inamaanisha kuwa watoa huduma za nyumba hawapaswi kukunyima nyumba au kukubagua kwa sababu ya vigezo vyovyote kati ya hivi.

Wakati wa janga la ugonjwa wa virusi vya korona, sheria za haki ya nyumba zinaweza kukulinda kutokana na ubaguzi wa nyumba unaohusiana na ugonjwa wa COVID-19.

Watu wenye ugonjwa wa COVID-19 wenye dalili ambazo zinamzuia zaidi mtu kutekeleza shughuli muhimu za maisha, au walio na historia ya kuwa na ugonjwa wa COVID 19, au wanaokisiwa kuwa wana ugonjwa wa virusi vya korona, wanaweza kulindwa kutokana na ubaguzi wa nyumba kutokana na ulemavu. Sheria za haki ya nyumba zinawalinda pia watu kutokana na ubaguzi wa utaifa, ikijumuisha ubaguzi dhidi ya watu kutoka maeneo mbalimbali duniani yanayohusishwa na asili au milipuko ya ugonjwa wa COVID-19.

Chini ya Sheria ya Haki ya Nyumba, Watoa huduma za nyumba hawapaswi:

- Kukataa kukubali watu wanaotoka kwenye nyumba za watu wenye mahitaji maalum, bila ushahidi wa maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19, kulingana na ueneaji unaodhaniwa wa ugonjwa wa COVID-19 kwa watu wanaoishi katika nyumba hizo
- Kuuliza ikiwa una ulemavu unaokufanya uwe na uwezekano zaidi wa kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19
- Kuwaambia wapangaji wengine kuhusu ugonjwa au ulemavu wako
- Kukunyima nyumba kutokana na imani kuwa watu kutoka Uchina wana uwezekano zaidi wa kuwa na ugonjwa wa virusi vya korona
- Kukomesha mkataba wako wa upangaji wa nyumba kwa sababu uliita gari la wagonjwa wa dalili za ulemavu
- Kukutenga wewe na watu wengine wenye ulemavu katika maeneo maalum ya jengo ili kukulinda dhidi ya kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19
- Kuruhusu kunyanyaswa kwa mpangaji na mpangaji mwingine kutokana na dhana za uongo kuhusu utaifa na uambukizaji
- Kukomesha mkataba wako wa upangaji wa nyumba kwa sababu unaonekana kuwa mgonjwa na unadhaniwa kuwa na ugonjwa wa COVID-19

Watoa huduma za nyumba lazima:

Watengeneze nyumba zinazofaa (kufanya mabadiliko au kutotekeleza kanuni zao za kawaida) ambazo zinahitajika ikiwa una ulemavu (kwa mfano, kukuruhusu kuhamia kwa muda kwenye chumba cha kibinafsi kwenye nyumba yako ya watu wenye mahitaji maalum unayoishi baada ya kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19, ikiwa kipo)

Watoa huduma za nyumba wanaweza:

- Kuhitaji kuwa wakazi na wageni wote wafuate hatua za usalama wa umma zinazopendekezwa au zinazohitajika ili kuzuia kusambazwa kwa ugonjwa wa COVID-19, ikijumuisha kutokaribiana na wengine na kuvaa barakoa
- Kuwaambia majirani kuwa kuna mtu ambaye ameambukizwa ugonjwa wa COVID-19 kwenye jengo (lakini hawapaswi kufichua jina, nambari ya nyumba au maelezo mengine ambayo yanaweza kumtambulisha aliyeambukizwa)
- Kuuliza maswali yanayohusiana na dalili za ugonjwa wa COVID 19 baada ya kuruhusiwa kuingia kwenye nyumba au kuingia katika maeneo ya umma au ya watu wengi
- Kuhimiza wapangaji au wanaotuma maombi ya nyumba kujiripoti wenyewe kuwa wana ugonjwa wa COVID-19 au kuna uwezekano kuwa wameambukizwa virusi vya korona (lakini hawapaswi *kuwataka* wafichue maelezo hayo)
- Kuomba hati zinazoonyesha kuwa nyumba inahitajika kwa ajili ya ulemavu (lakini hawapaswi kuomba maelezo ya ugonjwa au ulemavu husika)